

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dodoma
29 Mei, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RAIS SAMIA AONGOZA KIKAO CHA KWANZA CHA TUME YA MIPANGO

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameongoza kikao cha kwanza cha Tume ya Mipango.

Tume hiyo imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Mipango Na.1 ya Mwaka 2023 na ina dhamana ya kusimamia Uchumi, upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Tanzania.

Kabla ya Kikao hicho Rais Samia aliwaapisha wajumbe sita wa Tume hiyo ambao ni Waziri wa Fedha Mhe. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Uwekezaji, Mhe. Prof. Kitila Mkumbo, Bw. Omar Issa, Balozi Ombeni Sefue, Balozi Ami Mpungwe na Balozi Asha-Rose Migiro.

Pamoja na mambo mengine, Rais Samia ameeleza kuwa Tume hiyo imebeba dhamana kubwa na imani yake ni kwamba itakidhi kiu na maratajio ya Watanzania katika kuwa na mipango ya pamoja na maendeleo jumuishi.

Aidha, ameitaka Tume ijitahidi kutathmini ubora wa miradi mbalimbali inayoendelea ili iwanufaishe wananchi kwa jumla na kutumia rasilimali chache kuleta matokeo makubwa.

Vilevile, Rais Samia amesisitiza umuhimu wa matumizi ya takwimu na tafiti kwenye kufanya maamuzi katika tume hiyo inayosaidiwa na Sekretarieti ya Tume ya Mipango ikiongozwa na Katibu Mtendaji.

Tume hiyo pia inawajibika kuandaa Mpango Mkakati ili kufungamanisha utekelezaji wa majukumu yake na Dira ya Taifa ya Maendeleo na kuishauri serikali kuhusu mipango ya maendeleo.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

